# Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI

# Kiambatisho 3: Sera ya Kuzuia Utumiaji wa Watu wengine Vibaya Kingono, Unyanyasaji wa Kingono au Udhalilishaji wa Kingono (PSEAH)

Mpango wa Upatikanaji wa Huduma za Afya wa Clinton ("CHAI") hauvumilii utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono. CHAI inajiunga na mashirika ya kimataifa yasiyo ya faida katika kuunga mkono kwa dhati kanuni za msingi kuhusu kuzuia utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono, zilizoanzishwa mwaka 2003 na Taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya Hatua Maalum. Tunaamini kwamba watu wote wana haki ya kuishi maisha yao bila ya unyanyasaji wa kingono.

Sera hii inatumika kwa wafanyakazi wote wa CHAI, kwa wakati wote, katika ushirikiano wao na wanufaishwa na umma. (Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI unajumuisha mienendo mipotovu ya kingono dhidi ya wafanyakazi wa CHAI, au dhidi ya wafanyakazi wa mashirika ya kiserikali au yasiyo ya kiserikali yanayoshirikiana na CHAI; tafadhali angalia sehemu ya Kukuza na Kudumisha Mazingira ya Kiheshima Kazini.)

Ni sharti wafanyakazi wote wa CHAI wazingatie mambo yafuatayo:

- Kuishi kwa njia ya uadilifu, kuwatendea watu wote kwa hadhi na heshima na kujiepusha na kufanya vitendo vyovyote vya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono.
- Kuchangia kwa mazingira ambayo wafanyakazi wote na wanufaishwa wana uwezo wa kutambua tabia isiyokubalika na kujihisi kuwa na uwezo wa kujadili haki na wasiwasi wao. Wasimamizi wana jukumu maalum la kudumisha mazingira haya.
- Kuibua maswala haraka iwezekanavyo, kwa mujibu wa taratibu za utoaji wa taarifa zinazofaa, kuhusu kesi yoyote ya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono.
- Kushirikiana kikamilifu na uchunguzi wowote wa CHAI, kwa kuheshimu ufaragha wa wote wanaohusika na kwa kuzingatia haswa uhuru na masilahi ya waathirika.

## Yaliyomo


I. Wajibu na Kusudi
II. Faharasa
III. Viwango vya Maadili vya Wafanyakazi
IV. Utekelezaji na Ufuatiliaji

V. Kutoa Taarifa za Malalamiko na Matatizo
VI. Hakuna Kulipiza Kisasi
VII. Uchunguzi

## I. Wajibu na Kusudi

Kazi ya CHAI huwafanya wafanyakazi wake kushirikiana na aina tofauti ya wanufaishwa na watu wengine, ikiwa ni pamoja na watoto na watu wanaoishi katika mazingira hatarishi. Kazi ya CHAI pia inaweka wafanyakazi wengi katika nafasi za uaminifu na mamlaka, hasa wakati wa udhibiti wa rasilimali na ugavi wa rasilimali.

Madhumuni ya sera hii ni kujenga mazingira salama kwa wanufaishwa na wananchi, na kulinda watoto na watu wazima wanaoishi katika mazingira hatarishi kutokana na madhara yoyote ambayo yanaweza kusababishwa na kushirikiana kwao na CHAI. Sera hii inalenga pia kuanzisha taratibu za kukabiliana na matukio ya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono, na kuwajulisha wafanyakazi kuhusu majukumu yao ya mkataba na maadili ya kulinda watoto na watu wazima wanaoishi katika mazingira hatarishi katika nyanja zote za kazi ya CHAI.

Sera hii ni sehemu ya Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI na imepitishwa na Timu ya Viongozi wa Ngazi ya Juu ya CHAI na Baraza la Wakurugenzi. Mkurugenzi Mkuu wa Rasilimali Watu wa CHAI anafanya kazi kama Kiongozi Mkuu wa Kuzuia Utumiaji wa Watu Wengine Vibaya Kingono, Unyanyasaji wa Kingono na Udhalilishaji wa Kingono na ana wajibu wa kuhakikisha utekelezaji na ufuatiliaji wa sera hii, pamoja na uangalizi kutoka kwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa CHAI.

## II. Faharasa

**Madai:** malalamiko rasmi kuhusu uwezekano wa uvunjaji wa Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI na mmoja wa wafanyakazi.

**Mnufaishwa**: mtu, kando na mfanyakazi mwingine wa CHAI, ambaye anapata msaada kutoka kwa shughuli za CHAI na kwa hiyo ana nafasi ya kutegemea CHAI kwa kiwango fulani.

**Mtoto**: mtu yeyote chini ya umri wa miaka 18, bila kujali ufafanuzi wa nchi husika kuhusu wakati mtoto anapokua mtu mzima.

**Mlalamikaji:** mtu anayetoa malalamiko, ikiwa ni pamoja na mwathirika wa utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono na udhalilishaji wa kingono au mtu mwingine ambaye anajua makosa na anatoa ripoti / anawasilisha lalamiko hilo.

**Ushahidi:** habari zilizokusanywa wakati wa uchunguzi zinazothibitisha au zinazopinga madai fulani.

**Kiongozi:** mtu aliyechaguliwa na CHAI kuchukua majukumu maalum kuhusiana na PSEAH, ikiwa ni pamoja na kupokea malalamiko ya kesi za utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono.

**Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI:** mkusanyiko wa viwango vya tabia ambazo wafanyakazi wote wa CHAI wanalazimika kuzingatia.

**Mchunguzi:** mtu aliyeteuliwa na Kiongozi Mkuu wa CHAI au mteule wake kuchunguza malalamiko fulani. Mchunguzi anaweza kuwa mfanyakazi wa CHAI aliyepewa mafunzo au mchunguzi kutoka nje.

**Mbia:** wakala au shirika ambalo lina jukumu muhimu katika kusaidia katika kufanikisha mradi wa CHAI, hutekeleza jukumu muhimu la uratibu au hufanya shughuli kwa jina la CHAI.

**Unyanyasaji wa kingono[1]:** tendo halisi au tishio la kumuingilia mtu kimwili kwa namna ya kingono, iwe ni kwa kutumia nguvu au katika hali ya kulazimishwa.

**Utumiaji wa watu wengine vibaya kingono[2]:** Tendo lolote halisi au jaribio la utumiaji vibaya wa nafasi ya udhaifu, mamlaka, au uaminifu kwa madhumuni ya ngono, ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu, kufaidika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na utumiaji wa mtu mwingine vibaya kingono.

**Udhalilishaji wa kingono**[3]: mapendekezo yoyote ya ngono yasiyokubalika, kudai rushwa ya ngono, mwenendo wa maneno au kimwili au ishara ya kingono, au tabia nyingine yoyote ya asili ya ngono, wakati, kwa mfano, mwenendo kama huo unaingilia kazi, huwa ni lazima ili kupewa kazi, au hukuza mazingira ya kutisha, ya chuki, au ya kukera. Udhalilishaji wa kingono unaweza kufanyika mtu akiwa karibu au mbali, ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu, kupitia simu, barua pepe, au mitandao ya kijamii. Ijapokua udhalilishaji hujidhihirisha katika mwenendo wa tabia, unaweza kuchukua mfumo wa tukio moja tu. Udhalilishaji wa kingono unaweza kutokea kati ya watu wa jinsia tofauti au watu wa jinsia moja. Watu wa jinsia zote wanaweza kuwa waathirika au wahalifu.

**Mwenendo mpotovu kingono:** kwa lengo la sera hii, mwenendo mpotovu kingono unahusu matendo ya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono kama ilivyoelezwa hapo juu.

**Mfanyakazi/mwajiriwa:** mtu anayefanyia kazi au kuwakilisha CHAI kwa wakati wote au kwa muda mchache, iwe analipwa au halipwi fedha zozote kwa ajili ya kazi kama hiyo au uwakilishi wake. Hii inajumuisha wafanyakazi wa kujitolea na watu wanaotumwa kwa kupendekezwa na watu wengine.

**Anayelengwa na malalamiko (SOC):** mtu anayetuhumiwa au kushukiwa kumtumia mwathirika vibaya kingono, kumnyanyasa au kumdhalilisha kingono.

---

[1] Chanzo: Taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (ST/SGB/2003/13).
[2] Chanzo: Taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (ST/SGB/2003/13).
[3] Chanzo: imetolewa kwenye Taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (ST/SGB/2008/5).

**Mwathirika:** mtu ambaye ametumiwa au alitumiwa vibaya kingono, kunyanyaswa au kudhalilishwa kingono.

**Shahidi:** mtu yeyote ambaye ana habari ambazo zinafaa kwa uchunguzi, ikiwa ni pamoja na mwathirika, mlalamikaji, mwajiriwa wa shirika lingine, anayelengwa na malalamiko au mwajiriwa mwingine.

## III. Viwango vya Maadili vya Wafanyakazi

Utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono na udhalilishaji wa kingono ni vitendo vya uovu, na *ukiukwaji wowote wa Viwango hivi unaweza kuwa sababu za kuchukuliwa kwa hatua za nidhamu ikiwa ni pamoja na kufutwa kazi mara moja.* Wafanyakazi wa CHAI wowote ambao wanafanya vitendo vya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono pia wanaweza kufunguliwa mashtaka ya jinai au kuchukuliwa hatua zingine za kisheria chini ya sheria husika.

1. Wafanyakazi wa CHAI hawapaswi kushiriki katika vitendo vya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono au kufaidika kimakusudi kutokana na matendo ya kuwatumia watu wengine vibaya kingono. Kwa mfano, ikiwa mwajiriwa wa CHAI anatumia nafasi yake au mamlaka yake kudai rushwa ya ngono kwa ajili ya manufaa fulani, hilo ni tendo la kutumia watu wengine vibaya kingono.

2. Wafanyakazi wa CHAI hawapaswi kushiriki katika vitendo vya unyanyasaji wa kingono au kufaidika kimakusudi kutokana na matendo ya kuwatumia watu wengine vibaya kingono. Kwa mfano, mwajiriwa wa CHAI akitumia nguvu katika kushiriki vitendo vya ngono, hilo ni tendo la unyanyasaji wa kingono. Matendo kama hayo ni pamoja na, lakini sio tu kubusu au kupapasa-papasa mwingine hadi kutenda tendo ovu zaidi la unyanyasaji wa kingono.

3. Wafanyakazi wa CHAI hawapaswi kushiriki katika vitendo vya udhalilishaji wa kingono. Kwa mfano, ikiwa mwajiriwa wa CHAI atamtongoza mwingine kwa maneno au vitendo vya kimwili kinyume na mapenzi yake, kumfanyia mzaha wa asili ya kingono au kuongea au kuandika kuhusu vitendo vya kingono na/au kueneza uvumi kuhusu maisha ya ngono ya mtu, hayo ni matendo ya udhalilishaji wa kingono.

4. Matendo ya ngono na watoto (watu chini ya umri wa miaka 18) ni marufuku bila kujali umri ambapo mtu anachukuliwa kuwa ni mtu mzima au umri ambapo mtu anaweza kufanya maamuzi ya kushiriki ngono katika eneo husika. Mtu hawezi kujitetea kwa msingi wa kudai kwamba alidhani mtoto husika alikuwa ni mtu mzima.

5. Kutoa au kupeana fedha, ajira, bidhaa, au huduma kwa ajili ya rushwa ya ngono, au kutoa au kupanga matendo ya ngono ya mtu mwingine kama sehemu ya rushwa hiyo, ni marufuku kabisa, hata ikiwa ni baada ya saa za kazi. Hii inajumuisha kutoa au kupeana msaada kwa mnufaishwa, ikiwa kutatumika kama njia ya kulazimisha matendo ya ngono.

6. CHAI inakataza sana matendo yoyote ya ngono kati ya wafanyakazi wa CHAI na wanufaishwa wanaoingiliana moja kwa moja kwa ajili ya msaada wanaopata wanufaishwa, ambapo kutokuwepo kwa usawa katika mamlaka kunaweza kuhujumu uaminifu na uadilifu wa kazi ya CHAI. Mfanyakazi anaweza kushauriana na Kiongozi ili aelekezwe juu ya usahihi wa uhusiano fulani. (Ili kuepuka shaka, aya hii haihusu watu binafsi wanaofanya kazi katika mashirika yaliyo katika ubia na CHAI au mashirika ya serikali yanayopata msaada kutoka kwa shughuli za CHAI, ila kwa kiwango ambacho wao pia hupata msaada wa moja kwa moja kutoka kwa CHAI. Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI huongoza mwenendo kati ya wafanyakazi wa CHAI na watu kama hao.)

7. Ikiwa mwajiriwa wa CHAI anaanza kukua na wasiwasi au anashuku utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono wa mfanyakazi mwenzake, iwe ni CHAI au shirika lingine, lazima apige ripoti kuhusu taarifa hizo kupitia mojawapo ya taratibu za taarifa za malalamiko zilizotajwa hapo chini au katika sehemu ya *Kuzingatia Kanuni na Kutoa Taarifa za Malalamiko* ya Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI.

8. Wafanyakazi wa CHAI wana wajibu wa kukuza na kudumisha mazingira ambayo yanazuia utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono. Wasimamizi katika ngazi zote wanapaswa kusaidia na kuendeleza mifumo inayohifadhi mazingira hayo na kuchukua hatua mara moja kwa kukabiliana na wasiwasi wowote. Wasimamizi katika ngazi zote wanapaswa kufuata taratibu za kuripoti kuhusu masuala yaliyoripotiwa kwao.

Tafadhali angalia viwango vya mwenendo vinavyohusiana na ushirikiano miongoni mwa wafanyakazi wa CHAI wao kwa wao, vinavyohusiana na ushirikiano wa wafanyakazi wa CHAI na wafanyakazi wa mashirika yaliyo katika ubia na CHAI na mashirika ya serikali ambayo yanashirikiana na CHAI.

## IV. Utekelezaji na Ufuatiliaji

Madai yote ya uovu au tabia isiyofaa yatachunguzwa kwa haki na kwa mujibu wa sera na taratibu za CHAI. CHAI itafanya kila iwezalo kuzuia utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono na kulinda waathirika wakati matatizo yanatokea. Ili kutimiza jambo hili, CHAI imechukua hatua zifuatazo:

- Kuweka uangalizi wa juhudi za PSEAH, sera na taratibu kwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji ili kufuatilia ufanisi, kuripoti maendeleo, na kuboresha jitihada za kuzuia na kushughulikia utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono.
- Kuweka Mkurugenzi Mkuu wa Rasilimali Watu kama Kiongozi Mkuu katika CHAI wa kusimamia shughuli zinazohusiana na PSEAH na Viongozi wengine, wenye wajibu wa kuweka Viongozi na wachunguzi, kusimamia uchunguzi, na kutoa taarifa kwa Afisa Mkuu wa Uendeshaji, kwa Timu Kuu ya Uongozi (SLT), na kwa Baraza kama ifaavyo.

- Kwa kufuata sheria zinazohusika na kwa kadri ya uwezo wa CHAI, kuzuia wahalifu wa utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono kuajiriwa au kuajiriwa tena na CHAI. Hii inaweza kujumuisha matumizi ya historia na kumbukumbu za uhalifu.
- Kuchunguza madai ya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono yanayohusisha wafanyakazi wa CHAI kwa wakati unaofaa na kwa uweledi unaostahili, na kuhakikisha mchakato unaofaa kwa kadri ya uwezo wa CHAI. Wachunguzi watafanya kazi yao bila upendeleo kwa kuheshimu haki na adhima ya walalamikaji, waathirika, na walengwa wa malalamiko. Hii ni pamoja na matumizi ya taratibu sahihi za kuwahoji walalamikaji na mashahidi, hasa kwa watoto na ushirikishwaji wa watafiti wa kitaaluma au kupata utaalamu wa uchunguzi kama ifaavyo. CHAI itachukua hatua juu ya matokeo ya uchunguzi na kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotokana na uchunguzi huo yanatumiwa kuboresha sera na utekelezaji kama ifaavyo.
- Kutoa mafunzo thabiti juu ya mada zinazohusiana na PSEAH kwa wafanyakazi wote wa CHAI.
- Kujumuisha habari za sera za PSEAH katika makubaliano ya ushirikiano, katika makubaliano ya ufadhili na kuhitaji mashirika husika kuripoti kwa CHAI mara moja iwapo tabia yoyote inayoaminika kukiuka sera hii itaibuka.
- Kupitia upya sera hii mara kwa mara na kuiboresha.
- Kuwa na rasilimali za kutoa msaada wa dharura na usaidizi wa kisaikolojia kama ifaavyo na inayowezekana kwa waathirika na wengine walioathirika na utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono.

## V. Kutoa Taarifa za Malalamiko na Matatizo

Masuala yote kuhusu uovu halisi wa kingono au jaribio la uovu huo au uvunjaji wa sera hii lazima uripotiwe mara moja. CHAI itashughulikia malalamiko yoyote au mashaka ya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono, hata kama hii ni katika kiwango cha uvumi. Si lazima kuwe na ushahidi wa kuunga mkono madai yako ili upige ripoti. Ikiwa mtu anatatizwa na kitu alichoona au kusikika ambacho kinaweza kuonyesha ukiukaji wa sera hii, hiyo ni sababu ya kutosha ya kuwasilisha malalamiko.

Walalamikaji wanapaswa kuhisi kuwa wako salama kutoa ripoti, na kwamba wanasikilizwa, na kwamba hatua zinazostahili zinachukuliwa. CHAI ina nia ya kuhimiza na kuwezesha wafanyakazi wote na wanufaishwa kujitokeza na kuripoti mambo yoyote yanayowatatiza kwa kufuata taratibu rasmi haraka iwezekanavyo, ili kuwezesha mambo hayo yashughulikiwe kwa wakati unaofaa. Wafanyakazi na wanufaishwa wanapaswa kujihisi wajasiri kuhusu kutoa taarifa yoyote ikiwa ni pamoja na utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono - iwe ni ya zamani au ya sasa.

CHAI itachukua masuala yote kwa njia ya uzito na kwa ungalifu mkubwa. Wafanyakazi wanaweza kutoa ripoti bila kujulikana kama hawataki kujitokeza binafsi.

Malalamiko na masuala yanayotatiza yanaweza kuwasilishwa kwa njia moja au zaidi ya njia zifuatazo:

**Nambari ya usaidizi ya CHAI**
chai@integritycounts.ca
+1-866-921-6714 (Bila malipo Marekani)
+1-604-922-5953 (Kimataifa)
www.integritycounts.ca

- **Mfanyakazi wa CHAI anaweza kuwasiliana na meneja wake.**
- **Wasiliana na Kiongozi Mkuu wa CHAI au Kiongozi wa CHAI mwingine aliyechaguliwa.**
- **Wasiliana na Nambari ya Usaidizi ya CHAI.** Nambari hii ya usaidizi ni huduma ya mtu wa tatu ya “upigaji ripoti”ambayo inaruhusu watu kutoa ripoti za kesi za uovu (bila kujulikana au kwa jina). Ripoti kutoka kwa watu wasiyojulikana (wasiyotaja majina yao) zitachukuliwa kwa uzito sawa na zile ripoti ambapo watu wanajitambulisha wenyewe**.**

Kila mwajiriwa wa CHAI ana jukumu la kuripoti matukio yalitokelezwa na wafanyakazi wa CHAI au mashirika yaliyo katika ubia na CHAI ambayo yanayoshukiwa kuwa ya utumiaji wa watu wengine vibaya kingono, unyanyasaji wa kingono au udhalilishaji wa kingono.

Mtu yeyote anayetoa ripoti kwa malengo ya kudhuru (k.m., kudanganya kuhusu jambo fulani linalomtatiza) atachukuliwa hatua za kisheria, kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria husika.

## VI. Hakuna Kulipiza Kisasi

CHAI haiwezi kuvumilia aina yoyote ya unyanyasaji, kulipiza kisasi, uonevu, au matokeo mabaya ya ajira dhidi ya wahusika wowote wa CHAI ambao wanaelezea mambo yanayowatatiza au wanatoa malalamiko kwa lengo nzuri kwa mujibu wa sera hii ya Mwongozo wa Kimataifa wa Mwenendo na Maadili ya Kazi wa CHAI, au vinginevyo. Mambo yanayotatiza yanaweza kuripotiwa kwa lengo nzuri, hata kama anayetoa ripoti hiyo amekosea. Wafanyakazi wowote wa CHAI ambao watanyanyasa, watalipiza kisasi, watamuonea, au kuchukua hatua mbaya dhidi ya mtu ambaye ameripoti jambo linalomtatiza kwa lengo nzuri, watachukuliwa hatua za kisheria, kwa kiasi ambacho kinaruhusiwa na sheria husika, hata ikiwa ni pamoja na kufutwa kazi.

## VII. Uchunguzi

Jitihada zote zitafanywa kulinda ufaragha wa walalamikaji wote, watoaji wa ripoti na wanaolengwa na malalamiko husika. Ijapokua CHAI haiwezi kuthibitisha usiri kamili, taarifa kuhusu malalamiko na uchunguzi itatolewa tu kwa watu wanaohitaji kujua. Ikiwa anayelengwa na malalamiko ni mkurugenzi wa CHAI, kiongozi, au mfanyakazi wa Rasilimali Watu wa Kimataifa, kiongozi wa kupokea malalamiko atafuata taratibu za kuepuka kuwahusisha katika kesi hiyo wale ambao wanaweza kuwa na mgogoro wa kimasilahi.

Wakati na baada ya uchunguzi, mtu yeyote ambaye anajua ripoti au malalamiko lazima aheshimu

uzito wa suala hilo na haja ya kulinda utambulisho, ufaragha na sifa ya anayedaiwa kulengwa na malalamiko hayo, mlalamikaji, watoaji wa ripoti, aliyeathiriwa na mashahidi wowote. Watu ambao hawatashirikiani na uchunguzi au wanaovunja usiri wa uchunguzi watachukuliwa hatua za kisheria, kwa kiwango kinachoruhusiwa na sheria husika.

Viongozi wa CHAI na wachunguzi watachukua hatua zote za kutosha ili kulinda mlalamikaji, mwathirika wa madai, anayedaiwa kulengwa na malalamiko, mtoaji wa ripoti na mashahidi wowote dhidi ya kulipiziwa kisasi, na kudumisha usalama wao katika taratibu za uchunguzi.